WIZARA YA AFYA

HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA MWANANYAMALA

# TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

**Mganga Mfawidhi** wa **Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Mwananyamala** anawatangazia Watanzania wenye sifa ya kuomba na kujaza nafasi ishirini na sita (26) za ajira ya **Mkataba wa kujitolea,** kuleta maombi yao. Nafasi zinazotangazwa ni:-

**1. DAKTARI II Nafasi 6**

Mwombaji awe na Shahada katika fani ya Udaktari kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali, awe amesajiliwa na Baraza la Madaktari na awe na leseni hai.

**2. AFISA MUUGUZI MSAIDIZI II Nafasi 15**

Mwombaji awe na Stahahada ya Uuguzi kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali, vyeti vya uuguzi na ukunga na leseni hai.

**3. MSAIDIZI WA AFYA Nafasi 2**

Mwombaji awe na astashahada ya Msaidizi wa Afya katika fani ya Maabara kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali

**4. DEREVA II Nafasi 2**

Mwombaji awe na cheti chs kufsulu kidsto chs Nne na amehitimu mafunzo ya udereva kutoka katika chuo kinacho tambuliwa na Serikali na awe na leseni ya udereva daraja C

**5. FUNDI VIYOYOZI Nafasi 1**

Mwombaji awe amehitimu kidato cha Nne na awe amehitifu mafunzo ya ufundi Sanifu katika viyoyozi (AC) kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali

KAIMU MGANGA MFAWIDHI
HOSPITALI YA MWANANYAMALA
S. L. P 61665
DAR-ES-SALAAM

**SIFA ZA JUMLA**

1. Awe na umri usiozidi miaka 45 (Arobaini na tano)
2. Awe amefaulu Kidato cha Nne/Sita
3. Awe na Kitambulisho cha Uraia
4. Awe na wadhamini wawili wanaotambulika na Serikali ya Kijiji / Mtaa anapoishi.

**MASHARTI YA JUMLA**

Waombaji wote waambatishe nakala ya cheti cha kidato cha nne/sita, cheti cha taaluma, cheti cha kuzaliwa, maelezo binafsi (Curriculum Vitae). Waombaji watakaowasilisha "Result Slip" "Statement of Result" Provisional Result" au Transcripts **HAVITAKUBALIKA.**

***Maombi yote yatumwe kwa:-***

Mganga Mfawidhi,
Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Mwananyamala,
S.L.P 61665.
**DAR ES SALAAM.**

Mwisho wa kuleta maombi ni tarehe **08/9/2025**. Saa **9:30 alasiri**.

***Imetolewa na:-***

KAIMU MGANGA MFAWIDHI
HOSPITALI YA MWANANYAMALA
S.L.P 61665
DAR-ES-SALAAM

**MGANGA MFAWIDHI**
**HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA MWANANYAMALA**
**01/09/2025**